



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**



TAARIFA KWA UMMA

**KUHUSU RATIBA YA UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE KATIKA JIMBO LA
SERENGETI NA SIMANJIRO PAMOJA NA
UDIWANI KATIKA KATA 21 ZA TANZANIA BARA**

Tume ilipokea barua kutoka kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye kwa kuzingatia kifungu cha 37(3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, aliitaarifu Tume uwepo wa nafasi wazi ya Ubunge katika Majimbo mawili (2), Jimbo la Serengeti lililopo Halmashauri ya Serengeti Mkoani Mara na Jimbo la Simanjiro katika Halmashauri ya Simanjiro Mkoani Manyara kufuatia Wabunge wa Majimbo hayo Waheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, na James Ole Millya kujiuzulu kutoka kwenye Chama chao cha awali.

Vile vile, Tume imepokea taarifa kutoka kwa Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa ambaye kwa kutumia mamlaka aliyopewa chini ya Kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, aliitaarifu Tume uwepo wa nafasi wazi za Madiwani katika Kata 21 za Tanzania Bara. Nafasi hizo wazi zimetokana na sababu mbalimbali ikiwemo vifo na kujiuzulu.

Kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 37 (1) (b) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, pamoja na kifungu cha 13(3) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatoa taarifa kwa Umma kuhusu uwepo wa Uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Majimbo ya Serengeti katika Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti na Simanjiro katika Halmashauri ya Simanjiro Mkoani Manyara, pamoja na Udiwani katika Kata Ishirini na Moja (21) za Tanzania Bara.

Tume imepanga kuendesha Uchaguzi mdogo katika Jimbo la Serengeti na Simanjiro pamoja na Kata 21 kwa kuzingatia Ratiba ifuatayo:

1. Fomu za Uteuzi wa Wagombea zitatolewa kati ya tarehe 28 Oktoba hadi 03 Novemba mwaka huu.
2. Uteuzi wa Wagombea utafanyika tarehe 03 Novemba mwaka huu
3. Kampeni za Uchaguzi zitafanyika kuanzia tarehe 04 Novemba hadi tarehe 01 Desemba mwaka huu na
4. Siku ya Uchaguzi itakuwa ni tarehe 2 Desemba, mwaka huu.

Tunapenda kuvikumbusha Vyama vya Siasa na wadau wote wa uchaguzi kuzingatia Sheria, Kanuni, Maadili ya Uchaguzi, Taratibu, Miongozo na maelekezo yanayotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi wakati wa kipindi chote cha Uchaguzi huu mdogo.

Imetolewa leo tarehe 10 Oktoba, 2018.

Jaji (R) Semistocles S. Kaijage
MWENYEKITI
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

KATA ZILIZOWAZI

NA	MKOA	NA	HALMASHAURI	NA	KATA
1.	ARUSHA	1	Halmashauri ya Wilaya ya Arusha	1	Ilboru
				2	Mlanfarini
				3	Oldonyosambu
		2	Halmashauri ya Manispaa ya Arusha	5	Engutoto
				6	Olasiti
2.	Dodoma	3	Halmashauri ya Manispaa ya dodoma	7	Hazina
		4	Halmashauri ya Chamwino	8	Chinugulu
3.	KAGERA	5	Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba	9	Kasharu
				10	Nyakimbili
				11	Kishongo
		6	Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe	12	Chonyonyo
				13	Ihanda
4.	KIGOMA	7	Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe	14	Muhindawa
				15	Mnanila
6.	LINDI	8	Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea	16	Mnerongongo
7.	KILIMANJARO	9	Halmashauri ya Wilaya ya Siha	17	Ngarenairobi
8.	MARA	10	Halmashauri ya Wilaya ya Butiama	18	Kyanyari
9	MWANZA		Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe		Namilembe
10.	PWANI	11	Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga	19	Lukanga

NA	MKOA	NA	HALMASHAURI	NA	KATA
				20	Beta
11.	SINGIDA	12	Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni	21	Chikola